ipbes
Science and Policy for People and Nature




# Jukwaa la Sera na Sayansi Baina ya Serikali Mbalimbali kuhusu Bioanuwai na Huduma za Mfumo wa Ikolojia (IPBES)

***Taarifa:***

## ‘Tathmini ya Nexus’ Inashughulikia Migogoro ya Kimataifa Iliyosokotana ya Bioanuwai, Maji, Chakula, Afya na Mabadiliko ya Tabianchi
## Wataalam wa IPBES Wanatoa Majibu Mbalimbali kwa Faida za Juu Zaidi

## ‘Kuunganisha Masuala Moja Moja kupitia Maamuzi Jumuishi na Yenye Kurekebika

**Ripoti Imeratibiwa Kuzinduliwa Saa 1pm GMT Jumanne, tarehe 17 Desemba 2024**

***"Migogoro ya kimataifa ya bioanuwai, maji, chakula, afya na mabadiliko ya tabianchi mara nyingi huzidisha athari ya kila mmoja inaposhughulikiwa kando na kwa hivyo inapaswa kushughulikiwa kwa pamoja. Tathmini ya Nexus ni miongoni mwa kazi kabambe zaidi kuwahi kutekelezwa na jumuiya ya IPBES, ikitoa miitikio mbalimbali ambayo haijawahi kutokea ili kupeleka maamuzi na hatua mbali na suala moja. Migogoro inayotokea mfululizo inaweza kuungana na kuwa mingi, lakini mbinu ya kiungo inazingatia utegemezi kati ya migogoro hii na hutoa suluhisho kamili ambazo zinaweza kuboresha matokeo katika sekta na mifumo mbalimbali." - Prof. Paula Harrison, Kituo cha Ikolojia na Haidrolojia cha Uingereza, Mwenyekiti Mwenza wa Tathmini ya Nexus ya IPBES***

- **Inashughulikia uhusiano changamano kati ya vipengele kiungo vya bioanuwai, maji, chakula, afya na mabadiliko ya tabianchi**
- **Inatoa utabiri wa miingiliano ya baadaye kati ya migogoro hii hadi mwaka 2100 katika matukio kadhaa tofauti**
- **Inatoa machaguo thabiti mbalimbali ya mwitikio, kwa kuzingatia kuboresha faida kwa bioanuwai, maji, chakula, afya na mifumo ya tabianchi**
- **Inachunguza gharama za kutochukua hatua na kutoshughulikia migogoro mingi pamoja**
- **Itasaidia ufanikishaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu, Mfumo wa Bioanuwai wa Kimataifa wa Kunming-Montreal na Mkataba wa Paris**
- **Imeandaliwa na wataalamu bingwa 165 kimataifa kutoka nchi 57, kutoka maeneo yote ya ulimwengu**
- **Inatokana na marejeleo 6,500, miaka 3 ikiendelezwa, kwa gharama ya jumla ya zaidi ya dola milioni 1.5**
- **Itaongoza maamuzi ya watendaji na taasisi (kwa mfano, Serikali, asasi za raia, Watu Asili na jumuiya za mitaa na sekta binafsi) kusimamia, kuingiliana na, kushawishi na kuathiriwa na vipengele vya kiungo na mwingiliano wao**
- **Uzinduzi wa Vyombo vya Habari Uliopangwa: 17 Desemba 2024 saa 13:00 GMT/08:00 EDT/14:00 CET/15:00 CAT**
- **Mitandao ya Kijamii: @IPBES #NexusAssessment**

Siku ya Jumanne, tarehe 17 Desemba 2024, Jukwaa la Serikali Mbalimbali la Bioanuwai na Huduma za Mfumo wa Ikolojia (IPBES) linapanga kuzindua **Ripoti yake ya Tathmini kuhusu uhusiano kati ya bioanuwai, maji, chakula na afya,** katika muktadha wa mabadiliko ya tabianchi (inayojulikana kama "Ripoti ya Nexus"). Ripoti hiyo itakuwa na **maana na thamani ya moja kwa moja kwa mtu yeyote anayefanya kazi au kuripoti juu ya nyanja hizi**.

Ripoti **inaangazia fursa za kuchukua hatua ndani na nje ya vipengele vya kiungo** vya bioanuwai, maji, chakula, afya na mabadiliko ya tabianchi**, ikigundua utangamano na usawaziko** kati ya machaguo ya mwitikio yanayohusiana na kila mmoja. **Inaonyesha jinsi kushughulikia kipengele kimoja kunavyoweza kuathiri vingine, kwa njia chanya na vilevile hasi, pamoja na kutambua machaguo mbalimbali ya mwitikio na faida katika vipengele vingi, ambavyo vinaweza kuchukuliwa sasa ili kuboresha matokeo.**

Ripoti hiyo imekuwa **ikiendelezwa kwa zaidi ya miaka mitatu, kwa gharama ya jumla ya zaidi ya dola milioni 1.5 za Marekani**. Imeandaliwa na **wataalamu bingwa 165 wa kimataifa kutoka nchi 57, kutoka maeneo yote ya ulimwengu**, wakiongozwa na wenyekiti wenza wawili: Prof. Paula Harrison (Kituo cha Uingereza cha Ikolojia na Haidrolojia, Uingereza) na Prof. Pamela McElwee (Rutgers, Chuo Kikuu cha Jimbo la New Jersey, Marekani). Inatumia marejeleo 6,500 ambayo yanateka uanuwai wa ushahidi na maarifa kuhusu bioanuwai, maji, chakula na afya katika muktadha wa mabadiliko ya tabianchi, pamoja na makala ya kisayansi, ripoti za serikali na maarifa ya Wenyeji wa Asili na maeneo husika.
Ripoti hiyo itazingatiwa na inatarajiwa kuidhinishwa katika kikao cha kumi na moja cha Mkutano Mkuu wa IPBES (#IPBES11, 10-16 Desemba 2024). **Mkutano Mkuu wa IPBES unawakilisha karibu Serikali 150** zinazojitahidi kuimarisha kiolesura cha sayansi na sera kwa ajili ya bioanuwai na huduma za mfumo wa ikolojia. 'Muhtasari kwa Watunga Sera' unaoangazia ujumbe muhimu, matokeo na machaguo **umeratibiwa kuzinduliwa kwa vyombo vya habari vya mseto (ana kwa ana na mtandaoni) huko Windhoek, Namibia, Jumanne, tarehe 17 Desemba 2024 saa 13:00 GMT/14:00 CET/08:00 EST – angalia nyakati nyingine duniani kote hapa: https://bit.ly/3WxVkF1** ). **Kiungo cha matangazo ya wavuti ya moja kwa moja: www.ipbes.net)**

**Mchakato wa kuvipatia utambulisho vyombo vya habari kwa ajili ya uzinduzi utaanza Oktoba. Ili kupokea mwaliko wa kutambuliwa, waandishi wa habari na mashirika ya vyombo vya habari ambayo bado hayajawekwa kwenye orodha ya vyombo vya habari vya IPBES wanafaa kujisajili hapa: http://eepurl.com/hxkQgn (vyombo vya habari pekee tafadhali).**

IPBES, ambayo mara nyingi huelezewa kama 'IPCC kwa ajili ya Bioanuwai', ni chombo cha kimataifa cha sayansi na sera kilichopewa jukumu la kutoa ushahidi bora unaopatikana kwa watoa maamuzi, kwa ajili ya watu na mazingira ya asili.

## Vipengele muhimu vya Ripoti ya Nexus

Migogoro ya mazingira ya kimataifa inayohusiana na bioanuwai, maji, chakula, afya na mabadiliko ya tabianchi mara nyingi imeshughulikiwa binafsi, kwa michakato tofauti (kwa mfano, mikataba tofauti ya kimataifa au mashirika/mamlaka tofauti ya kitaifa). Vitendo vya kushughulikia mgogoro mmoja, kama vile mabadiliko ya tabianchi, mara nyingi vimezidisha matokeo mabaya ya migogoro mingine, hasa kuhusiana na bioanuwai. Kuna mkusanyo mkubwa wa maarifa ya kisayansi kuhusu kila mojawapo ya migogoro hii, lakini hakujawahi kuwa na utangamano muhimu wa kimataifa juu ya uhusiano kati ya migogoro hii hapo awali.

Huku ikijenga juu ya kazi iliyochapishwa na IPBES katika muongo mmoja uliopita, Ripoti ya Nexus:

- Inatoa muhtasari wa uhusiano wa sasa na mwingiliano kati ya vipengele vitano vya kiungo, ikichunguza ni nani aliyeathiriwa zaidi, aliye hatarini zaidi na anayefaidika zaidi na mwingiliano huu. Pia inatoa makadirio halisi ya gharama za kiuchumi za kushindwa kuchukua hatua na ya kushughulikia vipengele binafsi vya kiungo badala ya pamoja
- Inachunguza mwingiliano wa kiungo unaowezekana wa siku zijazo, ikikadiria matukio hadi 2050, lakini pia ikizingatia upeo wa hadi 2100 ili kuelewa vizuri changamoto na fursa za muda mrefu za kuchukua hatua ndani na kwenye vipengele vitano vya kiungo
- Inawasilisha machaguo anuwai ya mwitikio kwa sera na hatua jumuishi ambazo zitafaidisha vipengele vingi vya kiungo kwa wakati mmoja
- Inazingatia utawala ambao utafaa kwa madhumuni ya kufikia mustakabali wa haki na endelevu, ikitoa ramani ya barabara ya 'utawala wa kiungo'

## Muundo wa Ripoti ya Nexus

Ripoti ya Nexus inajumuisha **sura saba**, ambazo hutoa msingi wa kisayansi wa ujumbe muhimu wa ripoti. Sura hizo zinatoa:

1. Utangulizi wa kiungo, ukielezea mfumo na umuhimu wa sera ya tathmini, kufafanua vipengele vya kiungo na jinsi vinavyotegemeana
2. Mielekeo ya zamani na ya sasa katika miingiliano ya bioanuwai na maji, chakula, afya na mabadiliko ya tabianchi, kutathmini athari za mazingira, kijamii na kiuchumi
3. Makadirio ya baadaye ya miingiliano kati ya vipengele vya kiungo, kuchambua viendeshi vikuu vinavyolingana na malengo ya sera
4. Machaguo ya sera, siasa na kijamii katika kiungo ambayo yanaweza kuwezesha na kuchapusha mpito kwa mustakabali mbalimbali endelevu
5. Miitikio mbalimbali inapatikana ndani ya kila kipengele cha kiungo kwa ajili ya kutoa faida za kiungo chote
6. Machaguo ya kutoa mbinu endelevu kwa fedha za umma na binafsi kwa vipengele vinavyohusiana na bioanuwai vya kiungo
7. Muhtasari na uunganishaji wa machaguo, mapungufu ya maarifa na teknolojia na maendeleo ya uwezo na ramani ya mbinu kamili za kufanya maamuzi

## Matokeo yanayotarajiwa

Ripoti ya Nexus ya IPBES:

- Itawapa wafanya maamuzi, pamoja na watunga sera na uanuwai mkubwa wa washika wadau, pamoja na ushahidi, uchambuzi na machaguo bora yanayopatikana kuhusu uhusiano kati ya bioanuwai, maji, chakula na afya katika muktadha wa mabadiliko ya tabianchi
- Itaongoza maamuzi na hatua jumuishi zaidi ili kufanikisha SDG, Mfumo wa Bioanuwai wa Kimataifa na Mkataba wa Paris
- Itatambua na kusisitiza jukumu la watendaji tofauti katika kushughulikia changamoto za kimataifa

## Watathmini na hadhira

Ili kuhakikisha viwango vya juu zaidi vya usahihi, uaminifu na umuhimu wa sera, Ripoti ya Nexus ya IPBES imetathminiwa kwa kina kupitia mchakato wa tathmini wa nje ulio wazi, huku kukiwa na maelfu ya maoni ya tathmini ya nje yaliyowasilishwa na wanasayansi, wafanya maamuzi (ikijumuisha Serikali), watendaji na wamiliki wa maarifa ya Wenyeji wa Asili na maeneo husika.

Ripoti ya Nexus imeandaliwa kwa ajili ya wigo mpana wa wafanya maamuzi, ikijumuisha viongozi wa serikali na biashara, vikundi vya asasi za raia, Wenyeji wa Asili na jumuiya za maeneo husika.

## Podikasti ya IPBES

Ili kusikia zaidi kuhusu wigo, ukubwa na umuhimu wa Ripoti, sikiliza Kipindi cha 4 cha Podikasti ya IPBES, *Nature Insight* – kitakachopatikana kuanzia mwishoni mwa mwezi Novemba 2024 popote unapopata podikasti zako.

| RATIBA ya miaka 3 | |
|---|---|
| *Juni 2021* | Mkutano Mkuu wa IPBES, unaojumuisha wawakilishi wa Nchi wanachama wa IPBES, uliidhinisha '[ripoti ya mawanda]' inayoanzisha ramani ya tathmini. |
| *Februari 2023* | Wataalam wa nje walitathmini rasimu ya kwanza ya sura, huku maoni ya tathmini yakishughulikiwa katika rasimu zilizofuata na wataalam wa IPBES. |
| *Januari 2024* | Serikali na wataalam walitathmini rasimu ya pili ya sura na rasimu ya kwanza ya muhtasari kwa watunga sera. Maoni haya yameshughulikiwa katika maandishi ya mwisho na wataalam wa IPBES. |
| *Desemba 2024* | Kuzingatiwa kwa maandishi ya mwisho na Nchi wanachama katika kikao cha Mkutano Mkuu wa #IPBES11 ya Muhtasari kwa Watunga Sera mjini Windhoek, Namibia, ikifuatiwa na uzinduzi wa vyombo vya habari uliopangwa kufanyika tarehe 17 Desemba 2024. |

**Ukumbi wa uzinduzi: #IPBES11, Windhoek, Namibia, tarehe 17 Desemba 2024**

**Kwa habari za hivi punde, matangazo ya hivi karibuni, wito kwa wataalamu na kadhalika, jisajili leo kama mshika dau wa IPBES:** www.ipbes.net/stakeholders (mashirika ambayo si vyombo vya habari)

## Kuhusu IPBES

Likiwa na Serikali wanachama karibu 150, Jukwaa la Sayansi na Sera la Serikali Mbalimbali la Bioanuwai na Huduma za Mfumo wa Ikolojia (IPBES) ni chombo cha kimataifa kinachotathmini hali ya bioanuwai na michango ya mazingira ya asili kwa watu, kwa kujibu maombi kutoka kwa wafanya maamuzi na hutoa muhtasari wa machaguo ya siku zijazo kulingana na machaguo tofauti za kijamii na kiuchumi.

Dhamira ya IPBES ni kuimarisha sera na maamuzi kupitia sayansi, kwa ajili ya uhifadhi na matumizi endelevu ya bioanuwai, ustawi wa muda mrefu wa binadamu na maendeleo endelevu.

Kamati ya IPBES inaandaliwa na Serikali ya Ujerumani na iko kwenye chuo cha Umoja wa Mataifa huko Bonn. Maelfu kadhaa ya wanasayansi ulimwenguni kote huchangia kazi ya IPBES kwa kujitolea. Wanateuliwa na Serikali au mashirika yao na kuchaguliwa na Jopo la Wataalam wa Taaluma Mbalimbali la IPBES.

*Ripoti ya Tathmini ya Mchavusho ya IPBES, iliyotolewa mwaka 2016, ilikuwa katika lugha 18 na vyombo vya habari zaidi ya 1,300 katika nchi zaidi ya 80. Taarifa ya habari: http://bit.ly/2sq6gbQ*

*Ripoti za Tathmini za Kikanda za IPBES na Ripoti ya Tathmini kuhusu uharibifu na Urejesho wa Ardhi, zilizotolewa mwaka 2017, zilikuwa katika lugha 37 na vyombo vya habari zaidi ya 2,500 katika nchi zaidi ya 124. Taarifa za habari: http://bit.ly/2C0tnNu na http://bit.ly/2ylipyo*

*Ripoti ya Tathmini ya Kimataifa ya IPBES, iliyotolewa mwaka 2019, ilikuwa katika lugha 50 na vyombo vya habari zaidi ya 10,500 katika nchi zaidi ya 170. Taarifa ya habari: http://bit.ly/GlobalAssessment*

*Ripoti za Matumizi Endelevu ya Spishi Mwitu ya IPBES na Tathmini ya Maadili ya IPBES, zilizotolewa mwaka 2022, zilikuwa katika lugha 36 na vyombo vya habari zaidi ya 1,800 katika nchi zaidi ya 100. Taarifa za habari: https://bit.ly/IPBES_SUA na https://bit.ly/IPBES_VA.*

*Ripoti ya Tathmini ya Spishi Vamizi za Kigeni ya IPBES, iliyotolewa mwaka 2023, ilikuwa katika lugha 44, na vyombo vya habari zaidi ya 2,400 katika nchi zaidi ya 105. Toleo jipya: https://bit.ly/InvasiveMedia*

Kwa maelezo zaidi wasiliana na: media@ipbes.net www.ipbes.net

**Fuata IPBES:**

x.com/@IPBES
facebook.com/IPBES
youtube.com/ipbeschannel
linkedin.com/company/ipbes
instagram.com/ipbes_
threads.net/@ipbes_
bsky.app/profile/ipbes.bsky.social
mas.to/deck/@ipbes